# Makubaliano ya mkataba kati ya

# Carbon Tanzania na Vijiji vya Lugonesi, Mwese, Bujombe, Lwega, Kapanga, Mpembe, Katuma na Kagunga

Mkataba huu umeandaliwa chini ya Sheria ya Ardhi ya vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Mikataba ya mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Misitu ya 2002

**Tarehe** ...........08........... **Mwezi** .........OKTOBA.......... **Mwaka** .......2018.......

## Makubaliano hii ni kati ya:

**Carbon Tanzania,** ni kampuni teule iliyoanzishwa sio kwa dhumuni la kutengeza faida ambayo ni sehemu ya CT LTD, ambayo ni kampuni ya kitanzania, ilivosajiliwa chini ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Kiambatanisho na 1.)

**Halmashauri ya Kijiji** cha **Lugonesi, Mwese, Bujombe, Lwega, Kapanga, Mpembe, Katuma na Kagunga** kuanzia hapa itajulikana kama **"Vijiji"** kwa maana serikali ya Vijiji na mipaka yake, **kama** ilivyosajiliwa chini ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mkataba huu unahusu uanzishwaji wa mradi wa kuepukana na ukataji miti kwa ajili ya kupunguza utoaji wa hewa ya ukaa kwa ajili ya kupunguza matumizi yasiyokuwa endelevu na uharibifu wa ardhi ili kuwezesha uanzilishaji wa utoaji hewa ya ukaa kwa njia ya usimamizi wa Jumuiya ya Vijiji, inayowezeshwa kwa kupitia ubia kati ya **Carbon Tanzania na Vijiji.**

## 1. Nia na Majukumu

Madhumuni kwa ujumla ya mkataba huu ni kama ifuatavyo:

a) Kuwezesha **Vijiji** kupata mapato kutokana na mauzo halali, kisheria ya bidhaa yatokanayo na hewa ya ukaa ambayo ni bidhaa zisizo za mbao ya misitu, kutumika kwa manufaa ya faida kiuchumi na kijamii na kwa maendeleo ya jamii.

b) Kuhakikisha umiliki endelevu wa kimila na usimamizi wa ardhi na kulindwa na **Vijiji** kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji No 5 ya 1999, na sheria zingine husika, pamoja na sheria zingine za muhimu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c) Kuboresha hali ya kimazingira na kuhimiza matumizi endelevu ya maliasili kwenye **Vijiji** kutokana na mpango wa matumizi bora ya Ardhi na sheria ndogo.

d) Kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa na hivyo kuchangia katika juhudi za hali ya hewa duniani sambamba na sera ya taifa ya Tanzania.

e) Kuwawezesha **Vijiji** kupata mapato ya utoaji wa huduma za mazingira katika mfumo wa matokeo ya hewa ya ukaa kwa njia ya kuboresha mpango wa matumizi ya ardhi na usimamizi endelevu wa misitu.

### 1.1 Majukumu ya pamoja na ya jumla

a) Pande zote katika mkataba huu vinatakiwa kuheshimu Sheria ya Misitu ya 2002 na sheria zitakazaofuata baadae zinazohusiana na ulinzi, pamoja na usimamizi wa Misitu hapa Tanzania na kufanya shughuli zote kulingana na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Pande zote katika mkataba huu kukubaliana na kuzuia shughuli yoyote ambayo ni kinyume na mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji na sheria ndogo.

c) Pande zote katika mkataba huu vitakuwa na uangalifu na uaminifu, na kujitoa kwa nguvu zote ili kupunguza uhamisho wa shughuli ambayo ni kinyume na malengo ya mradi huu, hasa kutokubali kubadili ardhi ya Misitu kuwa ardhi ya kilimo, kwa maeneo ya karibu na nje ya eneo la mradi (Mchakato unaojulikana kama kuvuja).

d) Pande zote katika mkataba huu watajitoa kufuatilia jinsi kiasi ya hewa ya ukaa imehifadhiwa au kupotea ndani ya eneo la mradi.

e) Pande zote katika mkataba huu watajitoa kufuatilia mabadiliko ya kiuchumi na kijamii katika **Vijiji** na maeneo ya jirani kama matokeo ya mpango huo.

f) Pande zote katika mkataba huu wanaweza wakapitia na, kwa wakati inayotakiwa kukubali kurekebisha malipo ya matumizi na kama inavyohitajika kufikia malengo ya mradi.

g) Pande zote katika mkataba huu vitachukuwa hatua kuhakikisha kuwa wananchi wa **Vijiji** wanaelewa na kujua majukumu yao kuhusiana na mradi huu na wanapewa nafasi ya kushiriki kikamilifu.

## 1.2 Majukumu ya Carbon Tanzania

**Carbon Tanzania** kuanzia sasa itafanya yafuatavyo:

a) Kutoa huduma ya kitaalam, mafunzo na msaada kwa **Vijiji** kama inavyotakiwa kwa mafanikio ya utekelezaji wa pamoja wa mradi wa kaboni na Misitu, ikiwa ni pamoja na tathmini ya ramani, makazi, kipimo ya bidhaa za kaboni, na taratibu nyingine zinazohitajika na **Vijiji** kukidhi malengo yao ya usimamizi endelevu wa misitu.

b) Kuwa mshirika mzuri na mwaminifu na **Vijiji** katika mradi huo

c) Kupata wanunuzi sahihi kwa ajili ya hewa ya ukaa iliyohifadhiwa katika eneo la mradi kama matokeo ya jitihada ya **Vijiji.**

d) Kuwapa **Vijiji** ripoti kila baada ya miezi sita juu ya maendeleo ya mradi kupitia kamati husika na mikutano.

e) Kulipa **Vijiji** 50% ya mapato kutokana na uuzaji wa kaboni, ikiwa vijiji vitafuata mipango yao ya matumizi ya ardhi ya kijiji na sheria hivyo kupunguza uharibifu wa miti. Kutoka hii 50% ya **Vijiji, Vijiji** vinakubali kukata 10% iende wilayani.

## 1.3 Majukumu ya Vijiji

**Vijiji** kuanzia sasa itafanya yafuatavyo:

a) Kuhakikisha uboreshwaji wa matumizi ya ardhi kwa kupitia njia ya utekelezaji ya mpango wa matumizi ya ardhi na sheria ndogo iliyopitishwa na kukubaliwa, ambayo ulinda eneo la msitu kwa faida ya wanachama wote wa jamii na vizazi vijavyo.

b) Shiriki kwa uangalifu kuzuia ukataji wa miti, kupitia usimamizi bora wa misitu, ufuatiliaji na shughuli za utekelezaji kwa mujibu.

c) Kuchukua hatua kuhakikisha kwamba wanachama wa **vijiji** huelewa na kujua majukumu yao kuhusiana na mradi huu na wapewe nafasi yote ya kushiriki.

d) Kuacha kuuza hewa ya ukaa kwa mtu au chombo chochote kuhusiana na kipande kile cha ardhi husika kama inavyolindwa na masharti na mpango wa matumizi bora ya ardhi.

e) Kuhakikisha kuwa taarifa zote zinazotolewa kwa **Carbon Tanzania** chini ya makubaliano hayo ziwe zenye ukweli na usahihi, na kuwajulisha **Carbon Tanzania** kuhusu mabadiliko yoyote halali yatakayo sababisha taarifa kuwa bila ukweli au usahihi.

f) **Vijiji** vyote vinakubali kulinda maeneo yao ambayo yametengwa kama hifadhi ndani ya **vijiji** vyao kwa mujibu wa sharia ndogo ya kijiji kutokana na mpango wa matumizi bora ya ardhi.

## 2. Masharti ya Mkataba

Masharti ya Mkataba yako kama ifuatavyo:

### 2.1 Uhalali wa Mkataba

Mkataba huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka 30 (thelathini) kuanzia tarehe ya kusaini mkataba huu na itakuwa inaisha baada ya kipindi hiki cha miaka 30 (thelathini).

Pande zote zinaweza kuanzisha mjadala ili kubadili au kurekebisha mkataba huu kwa wakati wowote kwa ajili ya kuongeza au kupunguza tarehe ya kumaliza mkataba. Hata hivyo marekebisho yoyote halali au majadiliano mapya itafanyika kwa maandishi na kwa njia ya pande zote kuweka saini zao.

### 2.2 Marekebisho

Mkataba huu unaweza kufanyiwa marekebisho au kuboreshwa kwa maandishi kama pande zote mbili watakubaliana kwa njia ya kuweka saini ya pande zote, **Carbon Tanzania** na **Vijiji.**

### 2.3 Usuluhishi wa Migogoro

Katika mzozo wowote ambayo unaweza kutokea baina ya pande hizi mbili kuhusiana na mkataba huu, wahusika kutoka kwenye hizi mbili watakutana kujadili jinsi ya kutatua mgogoro. Kama upande mmoja itakuwa bado haijaridhika au kama vipande kushindwa kufikia makubaliano, watarejea mgogoro wao kwa Kamati ya Rufaa na Malalamiko. Kamati itakuwa na watu wafuatao.

1. Mwakilishi kutoka **Carbon Tanzania**.
2. Mwakilishi wa kuchaguliwa kutoka kila moja ya **vijiji** vinayvo shiriki katika mpango wa kuzuia ukataji miti.

3. Watu wawili wenye sifa utaalamu sahihi waliochaguliwa na pande zote mbili kusimama kwa niaba yao.

Upande wowote una haki ya kuleta mgogoro mahakamani baada ya kushindwa michakato ya hapo juu.

## 2.4 Masuala yanayozidi uwezo ya binadamu/ Nguvu za kiasili

Katika mkataba huu, hakuna upande utakaohusika kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake iwapo kushindwa huko ni kutokana na matokeo ya matendo ya asili kama vile; moto, mafuriko, tetemeko la ardhi na dhoruba, upepo au maafa asilia, vita, uvamizi, vita vya wenyewe, uasi, mapinduzi ya kijeshi au nguvu ya kuondolewa madarakani, shughuli za kigaidi, kutaifisha, serikali kuidhinisha, kufungana, vikwazo, kazi ya mgogoro, mgomo, kufungiwa nje.

Iwapo upande wowote, **Carbon Tanzania** au **Vijiji** utadai kuwa nguvu za kiasili *(Force majeure)* kama sababu ya kushindwa kutekeleza majukumu yake, utatakiwa kuthibitisha kuwa hatua zinazostahili zilichukuliwa chini ya mazingira ya wakati ule ili kupunguza kuchelewa au uharibifu unaosababishwa na matukio yanayoonekana.

Mkataba huu umesainiwa hapa chini na pande zote za mkataba huu zinazohusika na kushuhudiwa siku ya....03.......... katika mwezi wa ....OKTOBA........mwaka ....2018..... na imehitimishwa na katika vijiji vya
LUGONESI, MWESE, LWEGA, BUJOMBE, KAPANGA, MPEMBE, KATUMA
katika kata za ..TARAFA YA MWESE..katika wilaya ya....TANGANYIKA....

**A. Kwa niaba ya Carbon Tanzania**

1. Jina...MARC BAKER...Cheo...DIRECTOR...Saini...........

**B. Kwa niaba ya Kijiji Cha Lugonesi**

1. Jina...PETER N. LYAKONEA...Cheo...M/KIJIJI LUGONESI...Saini...........

2. Jina...DEODATUS P. KALOLO...Cheo...VEO...Saini...........

**B. Kwa niaba ya Kijiji Cha Mwese**

1. Jina...MORIS . SALUM...Cheo...M/KITI MWESE...Saini...........

2. Jina...DEVOTHA MBOSSO...Cheo...VEO...Saini...........

**B. Kwa niaba ya Kijiji Cha Bujombe**

1. Jina...MUSSA KINGA...Cheo...M/KITI...Saini...........

2. Jina...JUSTINA JOHN...Cheo...VEO...Saini...........

**B. Kwa niaba ya Kijiji Cha Lwega**

1. Jina...BENEDICTO KIBERENGE...Cheo...M/KITI...Saini...........

2. Jina...JOHN A. MPINA...Cheo...VEO...Saini...........

**B. Kwa niaba ya Kijiji Cha Kapanga**

1. Jina...DEUS HAWA...Cheo...M/KITI...Saini...........

2. Jina...SAID M. WAMBALI...Cheo...V.E.O...Saini...........

**B. Kwa niaba ya Kijiji Cha Mpembe**

1. Jina...ABDALAH JUMA...Cheo...M/KITI KIJIJI...Saini...........

2. Jina...WILBROD SIMON...Cheo...VEO...Saini...........

**B. Kwa niaba ya Kijiji Cha Katuma**

1. Jina...YASINI H. KAPAYA...Cheo...MW/KITI KIJIJI...Saini...........

CT LIMITED
P.O. BOX 2428 ARUSHA
www.carbontanzania.com

MW/KITI WA KIJIJI LUGONESI

HALMASHAURI YA KIJIJI CHA BUJOMBE S.L.P MPANDA

MWENYEKITI WA KIJIJI LWEGA.

M/KITI WA KIJIJI KAPANGA

MW/KITI S- KIJIJI KATUMA

2. Jina THEOFRIDO EDWORD Cheo VEO Saini [signature]

**B. Kwa niaba ya Kijiji Cha Kagunga**

1. Jina JUMANNE L. NA... Cheo M/KITI KIJIJI Saini [signature]
2. Jina EDSON B. MPANGALA Cheo VEO Saini [signature]

**D. Kushuhudiwa**

1. Jina MBUKI A. JOHN Cheo AFISA USHIRIKA II Saini [signature]

2. Jina SALEHE M. MHANDO Cheo DC Saini [signature]

MKUU WA WILAYA TANGANYIKA